# UCHAGUZI MKUU WA MAISHA YANGU MWAKA 2020.

***"Mimi ................................................ nimejichagua kuwa kiongozi mkuu wa maisha yangu, maisha yangu ni jukumu langu na nitachukua hatua kuhakikisha yanakuwa bora.***

***Kila siku nitakazana kuwa bora zaidi ya nilivyokuwa jana, kila siku nitajifunza kitu kipya na nitajituma kwa kwenda hatua ya ziada kwenye kila ninachofanya.***

***Kila siku nitakazana kukuza kipato changu zaidi kwa kukazana kutoa thamani kubwa zaidi kwenye kile ninachofanya.***

***Kwa kila kipato ninachoingiza, asilimia 10 nitajilipa mimi mwenyewe kwa kuweka akiba sehemu ambayo siwezi kuitumia na baadaye nitawekeza akiba hiyo ili izalishe zaidi.***

***Kila kinachotokea kwenye maisha yangu nitakitumia kwa manufaa zaidi, sitalalamika wala kumlaumu yeyote, kama kuna kitu sikipendi nitakibadili na kama siwezi kukibadili nitaachana nacho.***

***Haya ndiyo maisha niliyochagua kuyaishi kwa miaka mitano ijayo na kila siku nitajikumbusha hili kabla ya kuanza siku yangu."***

............................................ (sahihi) .............................(tarehe)